# TOLEO LA TAKWIMU ZA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA KWA WANAWAKE NA WATOTO -ZANZIBAR, JUNI MWAKA 2022

**Na: 06**

*Office of Chief Government Statistician*

*P.O. Box 2321, Zanzibar*
Telephone +255242231869
Email: zanstat@ocgs.go.com
Website: http://www.ocgs.go.tz

*Police Headquarter Zanzibar*

P.O.Box 237, PHQ Zanzibar
Fax No: 024223136
Email:cidhqznz@gmail.com

**Utangulizi**
Ofisi ya Mtakwimu Mkuu imeandaa utaratibu ambao utawezesha ofisi kutekeleza majukumu yake iliyojipangia kuimarisha takwimu za jinsia. Miongoni mwa takwimu hizo ni kukusanya takwimu za matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia.

Toleo hili hutolewa kila mwezi ambalo hutoa muhtasari wa takwimu za maeneo mawili ya uhalifu ambazo ni ukatili na udhalilishaji wa kijinsia. Takwimu hizi zinatolewa kwa kutofautiana kwa kijiografia, kimakundi na kijinsia.


Takwimu za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia hutoa taarifa za idadi ya matukio yaliyotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia. Takwimu hizo hutoa taarifa kuhusu matukio ambayo yameainishwa katika makundi makuu sita (6).

**Lengo**
Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia za ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu na hutumiwa na wapangaji, watunga sera, na watoa maamuzi.

**Matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia**

Jumla ya matukio 97 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa mwezi wa Juni, 2022. Kulikuwa na waathirika 97 ambao waathirika Wanawake ni 12(asilimia 12.4) na watoto ni 85 sawa na asilimia 87.6, miongoni mwao wasichana ni 63(asilimia 74.1) na wavulana ni 22 (asilimia 25.9).


**Kielelezo 1.1: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, Juni 2022**




**Chanzo: Makao** makuu ya Polisi –Zanzibar

Wilaya ya Kati imeripotiwa kuwa na matukio mengi ukilinganisha na wilaya nyengine (matukio 19), ikifuatia Wilaya ya Magharibi "B" ambapo kumeripotiwa matukio 14. Wilaya ya Kusini na Mkoani zimeripotiwa kuwa na idadi ndogo ya matukio kuliko wilaya zote (matukio matatu (3) kwa kila wilaya).

**Kielelezo 1.2: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya, Juni 2022**




**Chanzo:** Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

Mlinganisho wa idadi ya matukio kwa mwezi imeongezeka kwa asilimia 31.1 kutoka matukio 74 kwa mwezi wa Mei, 2022 hadi 97 mwezi wa Juni, 2022. Aidha, Wilaya ya Magharibi "A" iliongoza kwa idadi kubwa ya matukio kwa Mei 2022 (matukio16) na Wilaya ya Kati imeongoza kwa idadi kubwa ya matukio kwa Juni 2022 (matukio19). Wilaya ya Kusini na Micheweni ziliripotiwa kuwa na idadi ndogo ya matukio kuliko wilaya zote (tukio moja (1) kwa kila wilaya) kwa mwezi Mei 2022.Wilaya ya Kusini na Mkoani zimeripotiwa kuwa na idadi ndogo ya matukio kuliko wilaya zote (tukio matatu (3) kwa kila wilaya) kwa mwezi Juni 2022.

**Jadweli 1.1: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya, Mwezi Mei na Juni 2022**

| Wilaya | Idadi ya matukio | | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume na maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Shambulio | |
| | Mei 2022 | Juni 2022 | Mei 2022 | Juni 2022 | Mei 2022 | Juni 2022 | Mei 2022 | Juni 2022 | Mei 2022 | Juni 2022 | Mei 2022 | Juni 2022 | Mei 2022 | Juni 2022 |
| Kaskazini 'A' | 2 | 4 | 1 | 1 | 1 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 5 | 8 | 4 | 5 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 |
| Kati | 8 | 19 | 6 | 4 | 0 | 9 | 1 | 1 | 0 | 4 | 1 | 1 | 0 | 0 |
| Kusini | 1 | 3 | 1 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Mjini | 12 | 7 | 6 | 3 | 0 | 1 | 1 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 | 0 |
| Magharibi 'A' | 16 | 13 | 3 | 6 | 4 | 3 | 4 | 2 | 1 | 0 | 0 | 2 | 4 | 0 |
| Magharibi 'B' | 10 | 14 | 2 | 7 | 1 | 2 | 0 | 2 | 1 | 2 | 1 | 1 | 5 | 0 |
| Wete | 10 | 10 | 5 | 4 | 0 | 0 | 1 | 0 | 2 | 1 | 2 | 0 | 0 | 5 |
| Micheweni | 1 | 4 | 1 | 3 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 5 | 12 | 3 | 3 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 6 | 0 | 0 |
| Mkoani | 4 | 3 | 2 | 3 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **74** | **97** | **34** | **40** | **9** | **20** | **7** | **10** | **4** | **9** | **6** | **12** | **14** | **6** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

Mlinganisho wa idadi ya matukio kwa mwaka ipo sawa kwa mwezi wa Juni 2021 na mwezi Juni 2022. Wilaya ya Magharibi "A" iliongoza kwa mwezi wa Juni, 2021(matukio 25) ambapo Wilaya ya Kati imeongoza kwa mwezi wa Juni, 2022 (matukio 19).

**Jadweli 1.2: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya, Mwezi Juni 2021 na Juni 2022**

| Wilaya | Idadi ya matukio | | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume na maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Shambulio | |
| | Juni 2021 | Juni 2022 | Juni 2021 | Juni 2022 | Juni 2021 | Juni 2022 | Juni 2021 | Juni 2022 | Juni 2021 | Juni 2022 | Juni 2021 | Juni 2022 | Juni 2021 | Juni 2022 |
| Kaskazini 'A' | 1 | 4 | 1 | 1 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 9 | 8 | 9 | 5 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Kati | 12 | 19 | 7 | 4 | 2 | 9 | 2 | 1 | 1 | 4 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Kusini | 1 | 3 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Mjini | 18 | 7 | 6 | 3 | 4 | 1 | 7 | 3 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 25 | 13 | 9 | 6 | 2 | 3 | 7 | 2 | 4 | 0 | 3 | 2 | 0 | 0 |
| Magharibi 'B' | 16 | 14 | 8 | 7 | 2 | 2 | 4 | 2 | 1 | 2 | 1 | 1 | 0 | 0 |
| Wete | 6 | 10 | 4 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 1 | 0 | 0 | 5 |
| Micheweni | 3 | 4 | 1 | 3 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 3 | 12 | 1 | 3 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 | 2 | 1 | 6 | 0 | 0 |
| Mkoani | 3 | 3 | 3 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **97** | **97** | **49** | **40** | **11** | **20** | **21** | **10** | **10** | **9** | **6** | **12** | **0** | **6** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

Miongoni mwa waathirika wa ukatili na udhalilishaji wa kijinsia waliobakwa ni 40, wanawake walikuwa watatu (3) na wasichana ni 37; Waliolawitiwa walikuwa 20, Kuingilia kinyume na maumbile ni 10 (wanawake walikuwa wawili (2) na wasichana walikuwa wanane(8)), Kutorosha walikuwa ni tisa (9) wote ni wasichana, shambulio la aibu walikuwa 12 (wanawake ni wawili(2), wasichana walikuwa nane (8) na wavulana walikuwa wawili (2)) na shambulio walikuwa sita (6) (wanawake ni watano (5) na msichana mmoja (1)).

**Jadweli 1.3: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Wilaya, Juni 2022**

| Wilaya | Idadi ya matukio | Aina ya ukatili na udhalilishaji Zanzibar | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kulawiti | Kuingilia kinyume na maumbile | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Shambulio | |
| | | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana |
| Kaskazini 'A' | 3 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 8 | 5 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kati | 18 | 3 | 9 | 1 | 4 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Kusini | 3 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Mjini | 7 | 3 | 1 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 13 | 6 | 3 | 2 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'B' | 13 | 6 | 2 | 2 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Wete | 5 | 4 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 10 | 3 | 1 | 0 | 2 | 0 | 4 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 3 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **85** | **37** | **20** | **8** | **9** | **0** | **8** | **2** | **1** | **0** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

**Jadweli 1.4: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake kwa Wilaya, Juni 2022**

| Wilaya | Idadi ya matukio | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kuingilia kinyume na maumbile | Kutorosha | Shambulio la aibu/Kukashifu | Shambulio |
| Kaskazini 'A' | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'B' | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Wete | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 |
| Micheweni | 2 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Chakechake | 2 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **12** | **3** | **2** | **0** | **2** | **5** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

Watoto wenye umri wa miaka 15-17 imeripotiwa kuwa na idadi kubwa ya matukio (matukio 42) sawa na asilimia 49.4 ya matukio yote ya watoto yalioripotiwa ikifuatiwa na umri wa miaka

11-14 (matukio 20) sawa na asilimia 23.5. Aidha matukio ya kubaka yanaonesha kuwa mengi zaidi katika umri wa miaka 15-17(matukio 32) sawa na asilimia 86.5 ya matukio yote ya kubaka yalioripotiwa.

**Jadweli 1.5: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Wilaya, Juni 2022**

| Miaka | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume na maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla |
| | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | |
| 0-5 | | 0 | 1 | | | 0 | 0 | 2 | 1 | 3 | 0 | 0 | 7 |
| 6-10 | | 1 | 9 | | | 2 | 0 | 0 | 1 | 3 | 0 | 0 | 16 |
| 11-14 | | 4 | 9 | | | 4 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 1 | 20 |
| 15-17 | | 32 | 1 | | | 2 | 0 | 6 | 0 | 1 | 0 | 0 | 42 |
| **Jumla** | | **37** | **20** | | | **8** | **0** | **9** | **2** | **8** | **0** | **1** | **85** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

Idadi ya watoto waathirika wa matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia kwa mwezi wa Juni, 2022 imeongezeka kwa asilimia 32.8 (matukio 85) ukilinganisha na mwezi wa Mei, 2022 (matukio 64). Mlinganisho wa idadi ya watoto waathirika wenye umri wa miaka 15-17 kwa mwezi uliopita imeongezeka kwa asilimia 44.8 kutoka matukio 29 kwa mwezi Mei 2022 hadi matukio 42 kwa mwezi wa Juni 2022.

**Jadweli 1.6: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Wilaya, Mwezi Mei na Juni 2022**

| Miaka | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume na maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla Mei 2022 | Jumla Juni 2022 |
| | Mei 2022 | Juni 2022 | Mei 2022 | Juni 2022 | Mei 2022 | Juni 2022 | Mei 2022 | Juni 2022 | Mei 2022 | Juni 2022 | Mei 2022 | Juni 2022 | | |
| 0-5 | 0 | 0 | 0 | 1 | 4 | 0 | 0 | 2 | 0 | 4 | 0 | 0 | 4 | 7 |
| 6-10 | 2 | 1 | 6 | 9 | 1 | 2 | 0 | 0 | 5 | 4 | 0 | 0 | 14 | 16 |
| 11-14 | 8 | 4 | 1 | 9 | 2 | 4 | 2 | 1 | 0 | 1 | 4 | 1 | 17 | 20 |
| 15-17 | 21 | 32 | 0 | 1 | 0 | 2 | 1 | 6 | 0 | 1 | 7 | 0 | 29 | 42 |
| **Jumla** | **31** | **37** | **7** | **20** | **7** | **8** | **3** | **9** | **5** | **10** | **11** | **1** | **64** | **85** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

Mlinganisho wa idadi ya watoto waathirika wenye umri wa miaka 15-17 kwa mwaka uliopita imepungua kwa asilimia 6.7 kutoka matukio 45 kwa mwezi wa Juni, 2021 hadi 42 mwezi wa Juni, 2022, ambapo matukio katika umri wa miaka 6-10 limeongezeka tukio moja kutoka matukio 15 kwa mwezi wa Juni 2021 hadi matukio 16 kwa mwezi Juni 2022.


**Jadweli 1.7: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Wilaya, Mwezi Juni 2021 na Juni 2022**

| Miaka | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume na maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla Juni 2021 | Jumla Juni 2022 |
| | Juni 2021 | Juni 2022 | Juni 2021 | Juni 2022 | Juni 2021 | Juni 2022 | Juni 2021 | Juni 2022 | Juni 2021 | Juni 2022 | Juni 2021 | Juni 2022 | | |
| 0-5 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 1 | 2 | 1 | 4 | 0 | 0 | 4 | 7 |
| 6-10 | 5 | 1 | 5 | 9 | 4 | 2 | 0 | 0 | 1 | 4 | 0 | 0 | 15 | 16 |
| 11-14 | 12 | 4 | 5 | 9 | 5 | 4 | 1 | 1 | 1 | 1 | 0 | 1 | 24 | 20 |
| 15-17 | 26 | 32 | 0 | 1 | 11 | 2 | 5 | 6 | 3 | 1 | 0 | 0 | 45 | 42 |
| **Jumla** | **44** | **37** | **11** | **20** | **20** | **8** | **7** | **9** | **6** | **10** | **0** | **1** | **88** | **85** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

Matukio 74 kati ya matukio 97 yanaonekana yametokea nyumbani sawa na asilimia 76.3 na matukio 23 yametokea sehemu nyengine sawa na asilimia 23.7.

**Kielelezo 1.3: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Sehemu Yaliyotokea, Juni 2022**




Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

Mlinganisho wa matukio yaliyotokezea sehemu nyengine kwa mwezi yameongezeka kwa asilimia 64.3 kutoka matukio 14 kwa mwezi wa Mei, 2022 hadi matukio 23 kwa mwezi wa Juni, 2022, ambapo matukio yaliyotokea nyumbani pia yameongezeka kwa asilimia 23.3 kutoka matukio 60 hadi matukio 74 kwa miezi hiyo.

**Jadweli 1.8: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Maeneo yaliyofanyika Matukio, Mei na Juni 2022**

| Eneo la matukio | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume na maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla Mei 2022 | Jumla Juni 2022 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Mei 2022 | Juni 2022 | Mei 2022 | Juni 2022 | Mei 2022 | Juni 2022 | Mei 2022 | Juni 2022 | Mei 2022 | Juni 2022 | Mei 2022 | Juni 2022 | | |
| Nyumbani | 25 | 30 | 6 | 15 | 6 | 10 | 4 | 7 | 5 | 6 | 14 | 6 | 60 | 74 |
| Kazini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Skuli/Madrasa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Sehemu nyengine | 9 | 10 | 3 | 5 | 1 | 0 | 0 | 2 | 1 | 6 | 0 | 0 | 14 | 23 |
| **Jumla** | **34** | **40** | **9** | **20** | **7** | **10** | **4** | **9** | **6** | **12** | **14** | **6** | **74** | **97** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

Mlinganisho wa idadi ya matukio yaliyotokea sehemu nyengine kwa mwaka uliopita yamepungua kwa asilimia 69.7 kutoka matukio 76 kwa mwezi wa Juni, 2021 hadi 23 mwezi wa Juni, 2022.

**Jadweli 1.9: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Maeneo yaliyofanyika Matukio, Juni 2021 na Juni 2022**

| Eneo la matukio | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume na maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla Juni 2021 | Jumla Juni 2022 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Juni 2021 | Juni 2022 | Juni 2021 | Juni 2022 | Juni 2021 | Juni 2022 | Juni 2021 | Juni 2022 | Juni 2021 | Juni 2022 | Juni 2021 | Juni 2022 | | |
| Nyumbani | 12 | 30 | 0 | 15 | 0 | 10 | 4 | 7 | 5 | 6 | 0 | 6 | 21 | 74 |
| Kazini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Skuli/Madrasa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Sehemu nyengine | 37 | 10 | 11 | 5 | 21 | 0 | 6 | 2 | 1 | 6 | 0 | 0 | 76 | 23 |
| **Jumla** | **49** | **40** | **11** | **20** | **21** | **10** | **10** | **9** | **6** | **12** | **0** | **6** | **97** | **97** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

Matukio 90 kati ya matukio 97 yaliyoripotiwa yapo chini ya upelelezi wa Polisi sawa na asilimia 92.8, matukio mawili(2) yapo Ofisi ya Mashtaka sawa na asilimia 2.1, matukio matatu (3) yapo mahakamani sawa na asilimia 3.1, tukio moja(1) limeachiwa huru na tukio moja(1) limefungwa na polisi sawa na asilimia 1.0 kwa kila tukio.


**Jadweli 1.10: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Hatua Zilizochukuliwa, Juni 2022**

| Aina ya matukio | Idadi ya matukio | Waathirika | | | Hatua zilizochukuliwa | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Wanawake | Watoto | | Zilizo Mahakamani | Zilizotiwa hatiani | Ziliachiwahuru | Zilizofungwa Polisi | Zilizopelekwa kwa Ofisi ya M' mashtaka | Zilizo chini ya Upelelezi wa Polisi |
| | | | Wasichana | Wavulana | | | | | | |
| Kubaka | 40 | 3 | 37 | | 1 | 0 | 1 | 0 | 1 | 37 |
| Kulawiti | 20 | | | 20 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 18 |
| Kuingiliwa kinyume na maumbile | 10 | 2 | 8 | | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 10 |
| Kutorosha | 9 | 0 | 9 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 8 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 12 | 2 | 8 | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 11 |
| Shambulio | 6 | 5 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 6 |
| **Jumla** | **97** | **12** | **63** | **22** | **3** | **0** | **1** | **1** | **2** | **90** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi -Zanzibar

Wafanyaji wa matukio ya ukatili na udhalilishaji wa Kijinsia walioripotiwa kwa mwezi wa Juni 2022 ni 97 wote walikuwa  ni wapita njia  sawa na asilimia 100.

**Kielelezo 1.4: Aina ya Watu Waliofanya Matukio ya Ukatiki na Udhalilishaji wa Kijinsia, Juni 2022**




Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

## Kiambatanisho

**Jadweli 1.0: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Maeneo yaliyofanyika Matukio, Juni 2022**

| Eneo la matukio | Kubaka | | | Kulawiti | | | Kuingilia kinyume na maumbile | | | Kutorosha | | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | | Shambulio | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla |
| Nyumbani | 30 | | 30 | | 15 | 15 | 10 | | 10 | 7 | 0 | 7 | 4 | 2 | 6 | 6 | 0 | 6 |
| Kazini | 0 | | 0 | | 0 | 0 | 0 | | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Skuli/Madrasa | 0 | | 0 | | 0 | 0 | 0 | | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Sehemu nyengine | 10 | | 10 | | 5 | 5 | 0 | | 0 | 2 | 0 | 2 | 6 | 0 | 6 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **40** | | **40** | | **20** | **20** | **10** | | **10** | **9** | **0** | **9** | **10** | **2** | **12** | **6** | **0** | **6** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

**Jadweli 2.0: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya, Juni 2022**

| Wilaya | Idadi ya matukio | Aina ya ukatili na udhalilishaji Zanzibar | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kulawiti | Kuingilia kinyume na maumbile | Kutorosha | Shambulio la aibu/Kukashifu | Shambulio |
| Kaskazini 'A' | 4 | 1 | 1 | 1 | 0 | 1 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 8 | 5 | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Kati | 19 | 4 | 9 | 1 | 4 | 1 | 0 |
| Kusini | 3 | 1 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Mjini | 7 | 3 | 1 | 3 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 13 | 6 | 3 | 2 | 0 | 2 | 0 |
| Magharibi 'B' | 14 | 7 | 2 | 2 | 2 | 1 | 0 |
| Wete | 10 | 4 | 0 | 0 | 1 | 0 | 5 |
| Micheweni | 4 | 3 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 12 | 3 | 1 | 0 | 2 | 6 | 0 |
| Mkoani | 3 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **97** | **40** | **20** | **10** | **9** | **12** | **6** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

**Jadweli 3.0: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, Mwezi Mei na Juni 2022**

| Aina ya matukio | Idadi ya matukio | | Waathirika | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Wanawake | | Watoto | | | |
| | | | | | Wasichana | | Wavulana | |
| | Mei 2022 | Juni 2022 | Mei 2022 | Juni 2022 | Mei 2022 | Juni 2022 | Mei 2022 | Juni 2022 |
| Kubaka | 34 | 40 | 3 | 3 | 31 | 37 | | |
| Kulawiti | 9 | 20 | | | | | 7 | 20 |
| Kuingiliwa kinyume na maumbile | 7 | 10 | 0 | 2 | 7 | 8 | | |
| Kutorosha | 4 | 9 | 1 | 0 | 3 | 9 | 0 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 6 | 12 | 1 | 2 | 2 | 8 | 3 | 2 |
| Shambulio | 14 | 6 | 3 | 5 | 3 | 1 | 8 | 0 |
| **Jumla** | **74** | **97** | **8** | **12** | **46** | **63** | **18** | **22** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

**Jadweli 4.0: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, Mwezi Juni 2021 na Juni 2022**

| Aina ya matukio | Idadi ya matukio | | Waathirika | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Wanawake | | Watoto | | | |
| | | | | | Wasichana | | Wavulana | |
| | Juni 2021 | Juni 2022 | Juni 2021 | Juni 2022 | Juni 2021 | Juni 2022 | Juni 2021 | Juni 2022 |
| Kubaka | 49 | 40 | 5 | 3 | 44 | 37 | | |
| Kulawiti | 11 | 20 | | | | | 11 | 20 |
| Kuingiliwa kinyume na maumbile | 21 | 10 | 1 | 2 | 20 | 8 | | |
| Kutorosha | 10 | 9 | 3 | 0 | 7 | 9 | 0 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 6 | 12 | 0 | 2 | 6 | 8 | 0 | 2 |
| Shambulio | 0 | 6 | 0 | 5 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **97** | **97** | **9** | **12** | **77** | **63** | **11** | **22** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

## Zingatia Maelezo

**Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia**

Kitendo chochote au mwenendo wowote, ambao husababisha moja kwa moja kwa mtu, kama mateso ya kimwili, ya kimapenzi au ya kiakili kupitia vitisho, kulazimisha au njia zingine; lengo la kutisha, kuadhibu, kuwadhalilisha, kudhoofisha usalama au kujiheshimu; kutosheleza hamu ya ngono; au kudhoofisha uwezo wa mwili au kiakili wa mtu kwa sababu ya jinsi yake. Kwa mfano, unyanyasaji wa kijinsia, kumpiga mke, unyanyasaji wa kijinsia wa wasichana na wavulana, ukeketaji wa kike, mwanamke kuua watoto wachanga, utoaji mimba, ukahaba wa kulazimishwa , Biashara haramu ya usafirishaji wa wanawake na watoto wa kike na ponografia (uenezaji wa ngono haramu).

Sheria ya Adhabu ya 6/2018 iliongeza adhabu kwa makosa yanayohusiana na maadili kama vile ubakaji, kulawiti, kuingilia kinyume na kimaumbile na shambulio la aibu;

Sheria hii imetungwa mwaka 2018 ambayo imekuja kufuta sheria kama hii ya mwaka 2004. Sheria hii imetungwa pamoja na mambo mengine kuyafanya baadhi ya matendo kuwa makosa ya jinai na kuyawekea adhabu zake endapo mtu yeyote atayatenda matendo hayo na mahkama itamuona ana hatia. Kwenye shehemu ya kumi na tatu (Section thirteen) ya sheria ya adhabu imejumuisha makosa mengi ambayo ni makosa dhidi ya vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto

Sheria ya mwenendo wa Jinai 7/2018 kifungu cha 151 (1) kina vifungu ambavyo haviruhusu utoaji wa dhamana kwa mtu yeyote anayeshtakiwa kwa kesi zinazohusiana na ukatili na udhalilishaji wa kijinsia, pamoja na kuongezeka kwa hukumu ambazo Mahakama zinaweza kupitisha. Kwa mfano, katika Mahakama ya Mkoa kesi za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia kutoka miaka 7 hadi miaka 14 na kwa Mahakama Kuu kutoka miaka 30 hadi kifungo cha maisha.

**Kwa ufafanuzi zaidi tafadhali wasiliana na:**

***Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali***
***Sanduku la barua, 2321***
***Barua pepe: zanstat@ocgs.go.tz***

***Makao Makuu ya Polisi Zanzibar***
***Sanduku la barua, 237, MMP, Zanzibar***
***Barua pepe:cidphqznz@gmail.com***